

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**BUNGE LA TANZANIA**

Tele: +255 026 2322761-5  
Fax No. +255 026 2324218  
E-mail: [info@bunge.go.tz](mailto:info@bunge.go.tz)



Ofisi ya Bunge  
S.L.P. 941  
DODOMA.

**TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI KUHUSU KUANZA KWA  
MKUTANO WA KUMI NA MOJA WA BUNGE**

---

Mkutano wa Kumi na Moja wa Bunge umepangwa kuanza kesho, siku ya Jumanne tarehe 3 Aprili 2018 na kumalizika tarehe 29 Juni 2018 Mjini Dodoma. Mkutano huu utakuwa ni mahususi kwa ajili ya mijadala na kupitisha Bajeti ya Serikali pamoja na kujadili Hotuba ya hali ya Uchumi wa Taifa itakayowasilishwa Bungeni na Waziri wa Fedha na Mipango. Aidha, Bunge litajadili utekelezaji wa Bajeti za Wizara zote kwa Mwaka wa Fedha 2017/18 na Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2018/19. Shughuli nyingine zitakazofanyika katika Mkutano huo ni kama ifuatavyo:-

**1.0 KIAPO CHA UAMINIFU**

Kutakuwa na Kiapo cha Uaminifu kwa Waheshimiwa Wabunge wawili waliochaguliwa katika uchaguzi mdogo uliofanyika hivi karibuni ambao ni:-

- i. Mhe. Maulid Abdallah Mtulia - Kinondoni
- ii. Mhe. Dkt. Godwin Oloyce Mollel - Siha

**2.0 UCHAGUZI WA WENYEVITI WA BUNGE**

Katika Mkutano huu wa Bunge, Bunge litafanya uchaguzi wa Wenyeviti watatu wa Bunge. Uchaguzi huu ni kutokana na Wenyeviti waliokuwepo kumaliza muda wao kwa Mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge.

### **3.0 MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI.**

Vilevile katika Mkutano huu wa Bunge, jumla ya Miswada ya Sheria miwili itawasilishwa Bungeni ambayo ni:-

- (i) Muswada wa Sheria ya Fedha za Matumizi wa Mwaka 2018 (The Appropriation Bill, 2018).
- (ii) Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2018 (The Finance Bill, 2018)

### **4.0 MASWALI.**

Katika Mkutano huu jumla ya Maswali ya kawaida 515 yanatarajiwa kuulizwa na kujibiwa Bungeni. Aidha, kwa mujibu wa Kanuni ya 38 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge wastani wa maswali 72 ya papo kwa papo kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu yataulizwa na kujibiwa kwa siku za Alhamisi.

### **5.0 MAAZIMIO.**

Bunge pia litajadili na kupitisha Azimio la Kuridhia Makubaliano ya Paris kuhusu Kuboresha Utekelezaji wa Mkataba wa Mabadiliko ya Tabia Nchi

Ratiba yote ya Mkutano wa Bunge inapatikana katika Tovuti ya Bunge ambayo ni [www.parliament.go.tz](http://www.parliament.go.tz)

Imetolewana:

Kitengo cha Habari, Elimu na Mawasiliano

Ofisi ya Bunge

**DODOMA**

2 Aprili, 2018.